

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA MITIHANI

MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

634

STADI ZA KAZI

Muda: Saa 3

Jumanne, 12 Mei 2015 mchana

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemmu A, B na C.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama 40, sehemu B na C zina alama 30 kila moja.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Bainisha madhara manne ya unyanyapaa katika elimu.
2. Taja mambo manne yanayounda muziki.
3. Changanua faida nne za kufanyia majoribio zana za kufundishia na kujifunzia **kabla** ya kutumika darasani.
4. Baini malighafi nne za asili zinazotengeneza vifaa vyaa ususi.
5. Kwa kutumia mifano anuai, elezea matumizi mawili ya vitafunwa katika **fani** ya upishi.
6. Taja aina nne za maswali yanayotumika katika majoribio ya darasani na mitihani ya somo la Stadi za Kazi.
7. Ukitoa sifa mbili, tofautisha kati ya rangi za maji na rangi za mafuta.
8. Orodhesha sehemu nne za baiskeli zinazoweza kuharibika.
9. Katika hoja mbili, elezea uhusiano uliopo kati ya matumizi ya zana za kufundishia na kujifunzia na kujifunza kwa mwanafunzi darasani.
10. Kwa kutumia hoja nne, taja umuhimu wa upimaji katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Eleza kanuni sita za msingi zinazopaswa kuzingatiwa wakati wa kupiga picha tuli.
12. “Mtaji ni kikwazo kwa wajasiriamali wengi wadogo hapa nchini”. Fafanua vyanzo vitano vya mtaji kwa mjasiriamali yeoyote anayetaka kuanzisha biashara.
13. Ukiwa kama mwalimu wa Stadi za Kazi katika Darasa la Tatu, chambua kanuni sita za ufugaji wa sungura.
14. Eleza faida nne na hasara mbili za usindikaji wa mboga na matunda.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

15. Eleza sababu tano za kuchambua muhtasari wa somo la Stadi za Kazi.
16. Changanua mbinu sita za kuzingatia katika kujenga mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi darasani.
17. Kuna umuhimu gani kwa mwali muhimu kutambua wanafunzi wenyewe matatizo ya nidhamu darasani kwake? Toa hoja tano.
18. Kwa kutumia hoja tano, eleza umuhimu wa kuandaa nukuu za somo kwa kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi.